Nuru ya Kiswahili, Juzuu 5(1), Juni 2026:93-118
DOI: https://doi.org/10.58548/2024nuru51.93118

# Uchambuzi wa Ukiushi wa Kisintaksia katika Tamthiliya ya *Mashetani*

**Felix Kwame Sosoo**
**Mhadhiri Mwandamizi, Chuo Kikuu cha Ghana**
fksosoo@ug.edu.gh

**Ikisiri**

Makala hii inafafanua dhana ya ukiushi wa kisintaksia katika tamthiliya ya *Mashetani* (1971) ya Ebrahim Hussein kama kisa mahsusi cha uchambuzi. Ukiushi hurejelea matumizi ya kimakusudi ya miundo inayokiuka kaida za kawaida za lugha ili kuibua athari za kimaana, kisaikolojia na kisanaa kwa hadhira. Ingawa dhana hii imejadiliwa kwa mapana katika taaluma ya elimumitindo, tafiti nyingi za Kiswahili zimejikita zaidi katika maudhui kuliko uchunguzi wa miundo ya lugha kama mbinu ya kisanii, hususan katika tamthiliya. Utafiti huu ulilenga kubainisha aina mbalimbali za ukiushi wa kisintaksia zilizotumiwa katika tamthiliya ya *Mashetani* na kueleza mchango wake katika kujenga dhamira za kazi husika. Tamthiliya iliteuliwa kwa kutumia usampulishaji lengwa kutokana na umahiri wake wa kimtindo na matumizi mapana ya lugha yenye ukiushi. Data zilikusanywa kwa njia ya usomaji wa matini na kuchanganuliwa kwa mkabala wa kitaamuli kwa kuongozwa na Nadharia ya Umtindo. Matokeo yanaonesha kuwa ukiushi wa kisintaksia ni mbinu muhimu ya kusisitiza maudhui na kuchochea tafakuri kuhusu masuala ya kijamii na kiitikadi. Makala hii inahitimisha kuwa uchambuzi wa miundo ya lugha ni muhimu katika kufichua maana za tamthiliya za Kiswahili na inapendekeza kuendelezwa kwa tafiti zaidi za kifani katika eneo hili.

**Dhana za Msingi:** Ukiushi, Tamthiliya, Umtindo, Isimu, Fasihi

## Utangulizi

Leech na Short (1981; 2007) wanaeleza kuwa ukiushi ni ukengeushi wa kimfumo kutoka katika kanuni za lugha unaojitokeza katika viwango mbalimbali kama vile sintaksia, semantiki na mofolojia. Kwa ujumla, ukiushi ni mbinu ya kimtindo inayotumiwa kwa makusudi na watunzi wa kazi za fasihi kwa kuvunja au kupotoka kutoka katika kaida za kawaida za lugha, miundo ya kisarufi na matarajio ya kimtindo ili kuzalisha athari mahususi za kimaana, kisaikolojia na kifasihi kwa hadhira.

Dhana ya ukiushi ina mizizi yake katika nadharia za wafomalisti wa Urusi, hususan kupitia hoja za Viktor Shklovsky aliyebainisha kuwa kazi kuu ya sanaa ni kuondoa mazoea ya upokeaji kwa kuifanya lugha na tajriba ya kawaida ionekane mpya au ngeni. Kwa mujibu wa Shklovsky (1965), mchakato huu wa ugenishaji huifanya lugha ya kifasihi ijitofautishe na lugha ya kawaida kwa kuvuruga matarajio ya msomaji au mtazamaji. Hivyo, ukiushi hauchukuliwi kama kosa la kisarufi bali kama mbinu ya kimakusudi ya kisanii inayolenga kuzalisha athari za kifikra na kihisia.

Wazo la ukiushi liliendelezwa na Mukarovsky (1977; 1990) kupitia dhana ya mchomozo, akieleza kuwa lugha ya fasihi hujitenga na matumizi ya kawaida kwa kuibua vipengele fulani vya lugha kupitia kuvunja ruwaza au kuvirudia kwa msisitizo. Katika mtazamo huu, ukiushi ni aina ya kuvuruga matarajio ya kiisimu kwa kuvunja kanuni za kawaida za kisintaksia, kimsamiati au kimantiki. Katika tamthiliya, mchomozo huwa na nguvu zaidi kwa sababu lugha haisomwi tu bali pia hutendwa jukwaani.

Kwa mujibu wa Cluysenaar (1976), ukiushi hujitokeza katika viwango mbalimbali vya lugha kama vile fonolojia, mofolojia, sintaksia na

semantiki. Hivyo, ukiushi si hitilafu ya bahati mbaya bali ni mbinu ya kisanii inayolenga kuzalisha maana ya ziada na kuamsha umakini wa msomaji au mtazamaji. Katika muktadha wa fasihi, ukiushi huchangia kuifanya lugha ionekane mpya na kuvunja mazoea ya upokeaji wa kawaida wa matini. Shklovsky (1965) anasisitiza kuwa kazi ya sanaa inalenga kuifanya lugha na tajriba ya kawaida ionekane mpya kupitia mbinu ya ugenishaji, hali inayomlazimisha msomaji kuitazama lugha kwa jicho jipya. Mukarovsky (1977) anaiendeleza dhana hii kupitia wazo la mchomozo, ambapo vipengele vya lugha huangaziwa kwa kuvunja au kurudia ruwaza za kawaida.

Katika miaka ya hivi karibuni, wataalamu wa Umtindo wameendelea kusisitiza umuhimu wa ukiushi katika ujenzi wa maana za kifasihi. Kwa mfano, Carter na Stockwell (2022) anaeleza kuwa ukiushi huifanya matini kuwa eneo la mwingiliano wa kiutambuzi kati ya mwandishi na msomaji kwa kuvuruga matarajio ya kawaida ya lugha. Vilevile, Burke (2021) anabainisha kuwa mbinu za mchomozo katika matini za kifasihi huongeza kiwango cha ushiriki wa kihisia na kiakili wa hadhira. Ukiushi wa kiisimu katika tamthiliya na riwaya husaidia kujenga tafsiri nyingi na kuifanya kazi ya fasihi kuwa wazi kwa usomaji tofauti kulingana na muktadha wa msomaji.

Mbinu ya ukiushi hutumiwa katika kazi za tanzu mbalimbali za fasihi, ikiwamo tamthiliya. Katika muktadha wa tamthiliya ya Kiswahili, wataalamu kama vile Ngara (1982) na Mwansoko (1991) wanaonesha kuwa ubunifu wa lugha ni msingi wa maendeleo ya fasihi, ingawa tafiti nyingi zimejikita zaidi katika maudhui kuliko uchunguzi wa miundo ya kisintaksia. Hivyo, ukiushi unaonekana si tu kama mbinu ya urembo wa lugha bali pia

kama nyenzo ya mabadiliko ya kifasihi na kijamii ndani ya utanzu wa tamthiliya.

Ukiushi wa kisintaksia, ambao ndio unaolengwa katika makala hii, unahusu uvunjaji wa kimakusudi wa mpangilio wa kawaida wa vipashio vya sentensi ili kuzalisha athari maalumu za kisanaa na kimaana. Katika matini za kifasihi, ukiushi huu unaweza kujitokeza kupitia miundo kama vile upinduzi wa sentensi, udondoshaji wa vipashio, takriri na usambamba unaokiuka matarajio ya kawaida ya lugha. Hivyo, ukiushi wa kisintaksia hauchukuliwi kama dosari ya kisarufi bali kama mkakati wa kimtindo unaomwezesha mwandishi kusisitiza dhamira na kujenga athari maalumu kwa hadhira.

Maendeleo ya fasihi, ikiwamo tamthiliya, hutegemea kuwapo kwa ubunifu wa lugha unaojumuisha ukiushi. Utanzu wa fasihi usio na ubunifu wa kimtindo hujikuta ukirudia miundo ileile na kupoteza mvuto wake wa kisanii. Uvunjaji wa kanuni za kawaida za lugha huwezesha matini za kifasihi kuwasilisha tajriba za kibinadamu kwa namna mpya na yenye nguvu zaidi ya kisanaa (Simpson, 2004). Kwa mantiki hiyo, ukiushi si mapambo ya lugha pekee bali ni kiini cha mageuzi na maendeleo ya utanzu wa kifasihi.

Hata hivyo, pamoja na mjadala mpana kuhusu ukiushi katika tanzu za riwaya na ushairi wa Kiswahili, tafiti nyingi hazijalenga kwa kina utanzu wa tamthiliya ambao unajengwa kwa misingi ya mazungumzo, migogoro ya moja kwa moja, na utegemezi wa jukwaa. Tamthiliya, tofauti na riwaya, huwasilishwa kupitia dayolojia na matendo ya wahusika, jambo linalofanya ukiushi wa kiisimu na kimuundo kuwa na athari ya haraka zaidi kwa

hadhira. Pengo hili la kiutafiti liliibua haja ya kuchunguza namna mbinu ya ukiushi inavyofanya kazi ndani ya tamthiliya za Kiswahili. Kwa kuzingatia hali hiyo, utafiti uliozalisha makala hii ulichunguza matumizi ya ukiushi wa kisintaksia katika tamthiliya ya *Mashetani* (1971) iliyoandikwa na Ebrahim Hussein.

**Kiunzi cha Nadharia**

Makala hii imejengwa juu ya Nadharia ya Umtindo ambayo huchunguza matumizi ya lugha katika matini za kifasihi kwa kuzingatia namna vipengele vya kiisimu vinavyozalisha maana, athari na dhamira. Chimbuko la nadharia hii linahusishwa na wafomalisti wa Urusi, hususan Viktor Shklovsky, ambaye katika insha yake ya mwaka 1917 alieleza kuwa sanaa hutumia mbinu ya kuifanya lugha iwe "ngeni" ili kuvunja mazoea ya upokeaji wa kawaida. Kwa mtazamo huo, lugha ya fasihi haipaswi kuwa ya moja kwa moja kama lugha ya mawasiliano ya kila siku, bali inapaswa kuamsha fikra kwa kuvuruga matarajio ya msomaji au mtazamaji. Dhana hii ina msingi mkubwa katika uchambuzi wa ukiushi kwa kuwa ukiushi ndio chombo kinachofanya mambo ya kawaida yaonekane mapya.

Kwa mujibu wa Leech (1969), Umtindo ni uchambuzi wa kisayansi wa matini unaounganisha isimu na uhakiki wa kifasihi. Anaonesha kuwa vipengele kama fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki havipo tu kama miundo ya lugha bali hutumika kama nyenzo za kisanii. Katika muktadha huu, ukiushi hufafanuliwa kama upotovu wa kimakusudi kutoka katika kaida za lugha, iwe katika mpangilio wa sentensi, uteuzi wa msamiati au matumizi ya miundo ya kisemantiki. Upotovu huo hauwi kosa bali huwa mkakati wa kimtindo unaolenga kuibua uchomozi na kusisitiza dhamira fulani.

Kuhusu maendeleo ya hivi karibuni ya Umtindo, Carter na Stockwell (2022) wanaonesha kuwa uchambuzi wa kimtindo unapaswa kuangalia namna vipengele vya lugha vinavyozalisha tajriba ya kiutambuzi kwa msomaji. Wanasisitiza kuwa ukiushi wa kisintaksia ni mojawapo ya mbinu muhimu zinazomwezesha mwandishi kuelekeza umakini wa msomaji katika sehemu mahususi za matini.

Aidha, wanaisimu wa Shule ya Prague kama Jan Mukarovsky walisisitiza kuwa lugha ya kifasihi hujitenga na lugha ya kawaida kwa kujenga uchomozi kupitia kurudiarudia, usambamba, au kuvunja ruwaza za kawaida za kisarufi. Hivyo, ukiushi unaweza kujitokeza katika ngazi ya fonolojia, mofolojia, sintaksia, na semantiki na kuathiri moja kwa moja tajriba ya hadhira. Kwa mfano, takriri au upinduzi wa sentensi huchelewesha upokeaji wa maana na kumlazimisha msomaji kuhusika kikamilifu katika ujenzi wa fasiri.

Katika makala hii, Nadharia ya Umtindo inatumika kufafanua namna ukiushi wa kisintaksia unavyojitokeza katika tamthiliya ya *Mashetani*. Kwa kuwa tamthiliya hujengwa kwa dayolojia na mazungumzo ya moja kwa moja, ukiushi katika utanzu huu huwa na athari ya haraka zaidi kisaikolojia na kiitikadi. Kupitia uchambuzi wa miundo iliyokiukwa, takriri na upinduzi wa sentensi, makala hii inaonesha kuwa ukiushi si suala la urembo wa lugha pekee bali ni mbinu mahususi inayotumika kufichua migogoro ya kitabaka, utambulisho wa nafsi na athari za ukoloni mamboleo.

## Methodolojia

Utafiti uliozalisha makala hii ulitumia mkabala wa kitaamuli. Utafiti ulijikita katika uchunguzi kifani kwa kuichagua tamthiliya ya *Mashetani*

(1971) iliyoandikwa na Ebrahim Hussein kama sampuli mahususi kwa sababu ni miongoni mwa tamthiliya za Kiswahili zilizoonesha ubunifu mkubwa wa kimtindo na matumizi ya lugha yenye mvuto na utata wa kisanii. Uteuzi wa tamthiliya ya *Mashetani* ulifanywa kwa kutumia mkabala wa usampulishaji lengwa ambapo kazi hiyo ilichaguliwa kwa makusudi kutokana na umahiri wake wa kipekee wa kimtindo, matumizi ya lugha ya kisanaa yenye ukiushi, na nafasi yake katika historia ya tamthiliya ya Kiswahili kama mojawapo ya kazi zinazojenga mjadala mpana kuhusu migogoro ya kijamii na kiitikadi katika jamii ya baada ya uhuru.

Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini wa matini ya tamthiliya husika. Mtafiti alisoma tamthiliya hiyo mara kadhaa kwa lengo la kubainisha vipengele vya ukiushi, hususan katika ngazi ya kisintaksia, kama vile takriri, upinduzi wa miundo ya sentensi, udondoshaji na matumizi ya miundo isiyo ya kawaida. Vipengele vilivyobainishwa vilinukuliwa na kupangwa kulingana na malengo ya makala ili kurahisisha uchambuzi wake. Katika uchambuzi wa data, mkabala wa kitaamuli ulitumika ambapo mifano ya matini ilifasiriwa kwa kina ili kubainisha namna vipengele vya ukiushi vinavyojenga dhamira katika tamthiliya. Matokeo ya uchambuzi yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo ya kifasihi na kiuchambuzi, yakihusisha mifano halisi ya matini pamoja na ufafanuzi wake katika muktadha wa Nadharia ya Umtindo.

Aidha, makala ilitumia data za upili zilizopatikana kupitia machapisho ya kitaaluma, vitabu, makala za majarida na tasnifu zinazohusu umitindo, ukiushi na uchambuzi wa tamthiliya za Kiswahili. Vyanzo hivyo vilipatikana katika maktaba na hifadhidata za kitaaluma, na vilisaidia kuimarisha mjadala wa kinadharia pamoja na kuweka matokeo ya utafiti

katika muktadha mpana wa taaluma ya fasihi na isimu. Ili kuongeza uhalali wa uchambuzi, data zilizopatikana zililinganishwa na hoja za wataalamu mbalimbali wa Umtindo na fasihi ya Kiswahili. Utaratibu huu uliwezesha matokeo ya utafiti kuwekwa katika muktadha mpana wa kitaaluma na kuimarisha mjadala kuhusu nafasi ya ukiushi katika ujenzi wa dhamira za tamthiliya za Kiswahili.

## Mwandishi na Muktadha wa Tamthiliya ya *Mashetani*

Ebrahim Hussein ni mwandishi wa kazi mbalimbali za fasihi, zikiwamo tamthiliya za Kiswahili. Alizaliwa mwaka 1943 nchini Tanzania na kujipambanua katika miaka ya 1960 na 1970 kama mwandishi aliyebadili mwelekeo wa tamthiliya kutoka katika maadili ya moja kwa moja hadi katika uchunguzi wa kifalsafa na kisaikolojia. Ni miongoni mwa wasanii na waandishi mashuhuri wa tamthiliya zilizojikita katika mbinu ya uchotarishaji. Ameandika tamthiliya nyingi, zikiwemo *Wakati Ukuta* (1967), *Kinjeketile* (1969) (kwa lugha za Kiswahili na Kiingereza), na *Mashetani* (1971). Ebrahim Hussein ni miongoni mwa waanzilishi wa tamthiliya ya kisasa ya Kiswahili. Kupitia tamthiliya kama *Kinjeketile*, *Mashetani*, *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi*, alionesha ubunifu wa hali ya juu katika matumizi ya ishara, falsafa na lugha yenye kina cha kimtindo. Katika kazi zake amedhihirisha umahiri wake katika uteuzi wa dhamira, ujenzi wa fikra na falsafa zinazodadisi jamii yake na pia anaonesha kuwa ni mjenzi na mtunzi huru wa tamthiliya. Mathalani, katika uteuzi wa dhamira Ebrahim Hussein anaibua matatizo na matukio yaliyomo ndani ya jamii na kujenga dhamira za ukombozi na harakati za mapinduzi na ukombozi wa wanyonge, ujenzi wa jamii mpya, mapinduzi ya kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Kwa kifupi, hajengi dhamira zake katika ombwe bali huitalii na kuianika

jamii inayomzunguka ili kutoa uelewa na ufahamu kwa wanajamii kuhusu maisha ya jamii. Anaitazama jamii yake ilivyo na kuona mwelekeo wake. Jambo hili pia linajenga falsafa yake.

## Maelezo Mafupi kuhusu Tamthiliya ya *Mashetani*

*Mashetani* (1971) ni mojawapo ya tamthiliya za Ebrahim Hussein zinazofafanua maisha ya jamii ya baada ya uhuru. Kazi hii inahusu migogoro ya kijamii, kitabaka na kisaikolojia kupitia wahusika wakuu, Juma na Kitaru, ambao wanawakilisha mitazamo tofauti kuhusu maisha na jamii. Kupitia migogoro yao, tamthiliya inaibua masuala ya utambulisho, mamlaka, usawa wa kijamii na athari za mabadiliko ya kijamii katika kipindi cha baada ya uhuru.

Tamthiliya ya *Mashetani* (1971) ni kazi inayochunguza mgogoro wa kitabaka, utambulisho wa nafsi na athari za mabadiliko ya kijamii katika Tanzania ya baada ya uhuru. Kazi hii inamzunguka Juma na Kitaru, wahusika wanaowakilisha matabaka mawili tofauti ya kijamii. Kupitia uhusiano wao, Hussein anafichua migongano ya kisaikolojia, kijamii na kiitikadi inayotokana na ukosefu wa usawa katika jamii. Miongoni mwa tamthiliya zake zinazodhihirisha umahiri huo wa kimtindo ni *Mashetani* (1971), ambayo imekuwa mojawapo ya kazi muhimu katika maendeleo ya tamthiliya ya Kiswahili ya kisasa. Tamthiliya hii inajengwa juu ya mgogoro wa kijamii, kisaikolojia na kiitikadi unaowakumba wahusika wake wakuu, Juma na Kitaru, ambao wanawakilisha matabaka mawili tofauti katika jamii ya baada ya uhuru. Kupitia mahusiano yao, Hussein anafichua athari za ukoloni mamboleo, migawanyiko ya kitabaka, mgogoro wa utambulisho wa nafsi na changamoto za mabadiliko ya kijamii.

Kwa kutumia ishara, taswira za kimajazi na lugha yenye ukiushi wa kimtindo, tamthiliya hii inaonesha jinsi watu wanavyoathiriwa na mifumo ya kijamii na kiuchumi inayozalisha ukosefu wa usawa, kutengwa na mkanganyiko wa kimaadili. Aidha, matumizi ya mazungumzo yenye utata, urudiaji wa miundo ya lugha na sentensi zilizovunjwavunjwa yanaifanya Mashetani*Mashetani* kuwa kazi inayofaa kuchunguzwa kwa mtazamo wa Umtindo, hususan katika kuchambua namna ukiushi wa kisintaksia unavyoshiriki katika kujenga dhamira za tamthiliya.

Moja ya mbinu aliyoitumia Hussein kufikishia dhamira zake ni uteuzi wa lugha. Usemaji na uteuzi wa misamiati maalumu, uchanganyaji ndimi ni miongoni mwa mbinu zilizojitokeza kwa wingi kiasi cha kujenga ukiushi ni miundo ya maneno na sentensi zake. Baadhi ya Wahakiki wamemlaumu mtunzi kwa kuijenga dhamira ya namna athari za ukoloni zinavyojitokeza katika kipindi cha baada ya uhuru miongoni mwa wanajamii kwa lugha ngumu.

**Aina za Ukiushi wa Kisintaksia katika Tamthiliya ya *Mashetani***

Katika tamthiliya ya *Mashetani*, Ebrahim Hussein anaonesha ustadi mkubwa katika matumizi ya ukiushi wa kisintaksia kama mbinu ya kisanii. Ilibainika kuwa lugha ya wahusika wake, mara nyingi, haifuati mpangilio wa moja kwa moja wa sentensi za Kiswahili sanifu, bali hujengwa kupitia miundo iliyovunjika, sentensi zisizo kamili, marudio yasiyo ya kawaida na mpangilio unaochelewesha au kupindua mtiririko wa kawaida wa kiima na kiarifu. Mbinu hizi hazitokei kwa bahati mbaya, bali zinahusiana kwa karibu na hali ya kisaikolojia ya wahusika, migongano ya ndani na nje, pamoja na mkanganyiko wa kijamii unaojitokeza katika jamii ya baada ya uhuru inayosawiriwa katika tamthiliya hiyo. Kwa hiyo, lugha inakuwa kioo

cha hali ya kiakili na kiitikadi ya wahusika badala ya kuwa chombo cha mawasiliano cha kawaida tu.

Kwa mfano, sentensi zilizokatika au zilizovunjwavunjwa huweza kuakisi msongo wa mawazo, hofu, mshangao au sintofahamu ya mhusika, huku upindishaji wa mpangilio wa kawaida wa sentensi ukitumiwa kusisitiza wazo au hali fulani ya kimaudhui. Hivyo, ukiushi wa kisintaksia katika *Mashetani* haupaswi kutazamwa kama upungufu wa kisarufi, bali kama mkakati wa kisanii unaobeba dhamira nzito za kijamii, kisiasa na kisaikolojia. Kwa ujumla, lugha si mfumo holela katika kazi hii, bali ni mfumo uliopangwa kwa makusudi ambapo kila mkengeuko una kazi ya kisanii.

Kwa ujumla, tulibaini kuwa mwandishi wa tamthiliya ya *Mashetani* ametumia aina nne za ukiushi wa kisintaksia kama mbinu ya kujenga maana za kifasihi. Aina hizo ni: takriri na usambamba, upinduzi wa sentensi, udondoshaji wa vipashio vya kisarufi, na urefushaji wa kauli. Aina hizi zinajadiliwa katika sehemu zinazofuata.

**Ukiushi wa kutumia takriri na usambamba**

Miongoni mwa aina za ukiushi wa kisintaksia zilizobainika katika tamthiliya ya *Mashetani* ni takriri na usambamba. Kwa kawaida, takriri na usambamba hutazamwa kama mbinu za uhusiano wa kimtindo zinazosaidia mshikamano wa matini, lakini katika muktadha wa tamthiliya hii, matumizi yake yanavuka kazi ya kawaida ya urembo wa lugha na kuingia katika eneo la ukiushi unaovunja uchumi wa lugha na matarajio ya mazungumzo ya kawaida. Hivyo basi, badala ya kuwa vipengele vya kurahisisha mawasiliano, vinabadilika na kuwa mbinu za kuunda mazingira ya kiishara,

kisaikolojia na kiitikadi yanayomlazimisha msomaji au mtazamaji kutafakari maana fiche iliyo nyuma ya muundo wa kauli. Mfano dhahiri wa takriri hii ya kiukiushi unajitokeza katika neno la kishetani "*Gashalazeritwas*," ambalo hurudiwarudiwa mara kwa mara katika usemezano kati ya Shetani na Binadamu. Kwa mtazamo wa kawaida wa kisarufi na kimawasiliano, kurudia neno moja bila maendeleo ya taarifa kunakiuka kanuni ya uchumi wa lugha, lakini katika muktadha wa kifasihi, urudiaji huo unalibeba neno hilo na kuligeuza kuwa kitovu cha maana. Neno hilo halitumiki kama kipashio cha kawaida cha lugha, bali linageuka kuwa kama tambiko au kauli ya kiuchawi yenye nguvu ya kiishara. Athari yake ni kuunda mdundo wa kimazingaombwe unaokaribiana na ibada, huku pia likijenga hali ya utegemezi na utii wa mhusika Binadamu kwa mamlaka ya Shetani.

Kwa mujibu wa Roman Jakobson (1960), urudiaji wa muundo katika matini huamsha kazi ya kishairi ya lugha, ambapo umbo la usemi hupata uzito sawa na maana yenyewe. Kwa msingi huu, "*Gashalazeritwas*" halipaswi kutazamwa kama neno la kawaida, bali kama muundo wa kisauti na kimaana unaobeba athari ya kiitikadi. Urudiaji wake unaimarisha mamlaka ya Shetani na kuunda mazingira ya hofu, ambapo lugha inakuwa chombo cha kudhibiti na kuathiri nafsi ya mhusika badala ya kuwa chombo cha mawasiliano tu. Hapa, takriri inafanya kazi ya kuvunja matarajio ya mazungumzo ya kawaida na kuunda aina ya lugha inayofanya kazi kama nguvu ya kisaikolojia.

Vivyo hivyo, kuna takriri ya maneno katika sehemu ya mazungumzo ya Kitaru kama inavyoonekana katika data inayofuata:

KITARU: "…yote yalianza katika kitendo. Kilianza kitendo, zikaja hadithi. Hadithi zikafanya mchezo ambao ni kitendo… ikiwa yote yalianza katika mchezo huu ambao ni kitendo… basi jawabu iko katika mchezo huu huu. Tukiucheza, na kuucheza, na kuucheza…" (uk. 56).

Katika dondoo hili, kuna maneno "kitendo" na "mchezo" yanayojenga usambamba wa kiukiushi unaojirudia bila kutoa mwelekeo wa moja kwa moja wa hoja. Pia, tunaona sentensi zinazojirudia na kukatika, zikirejea wazo lilelile kwa namna tofauti bila maendeleo ya kimantiki ya mstari wa hoja. Hali hii inaonesha kuvunjwa kwa kanuni za sintaksia ya kawaida, ambapo sentensi zinatarajiwa kuendelea kwa mpangilio wa mantiki na mshikamano wa mawazo. Badala yake, msomaji anakutana na mzunguko wa kauli unaojirudia, unaosababisha mkanganyiko wa kimtazamo na kumlazimisha kutafuta maana iliyo nyuma ya kurudiwarudiwa huko. Usambamba na takriri havifanyi kazi ya kuendeleza hoja kwa njia ya kawaida, bali vinajenga mzunguko wa fikra unaoonesha mkanganyiko wa kiitikadi. "Kitendo" kinabadilishwa kuwa "mchezo," na "mchezo" unarudi tena kama "kitendo," hali inayovunja mipaka ya uelewa wa moja kwa moja. Kwa mujibu wa Leech na Short (2007), ukiushi katika matini za kifasihi huibua mshikamano wa kimaana kwa njia isiyo ya moja kwa moja, ambapo msomaji hulazimika kujaza mapengo ya maana yaliyosababishwa na mkengeuko wa sintaksia. Hapa, usambamba wa kurudiarudia huleta athari ya kuchelewesha maana na kuimarisha tafakuri ya kina kuhusu uhusiano kati ya lugha, nguvu na jamii. Zaidi ya hapo, Van Peer (1986) anaeleza kuwa ukiushi katika lugha huongeza ushiriki wa kiakili wa msomaji kwa kuvunja matarajio ya kawaida ya usomaji.

Katika muktadha wa *Mashetani*, usambamba huu wa kurudia "kitendo," "mchezo" na "sumu" unachochea msomaji kuhusisha lugha na hali halisi ya kijamii inayooneshwa, ambapo kitendo cha kijamii kinageuka kuwa mchezo wa kiitikadi unaozaa athari hasi kwa jamii. Hivyo, "kitendo" kinapewa sura ya mchezo wa kijamii unaoathiri jamii kwa njia fiche, huku "sumu" ikiwa ni sitiari ya athari za ukoloni mamboleo na mifumo ya kiutawala inayowaweka watu katika hali ya utegemezi na kutojitambua.

Mbali na takriri ya maneno na miundo ya sentensi, Hussein pia anatumia takriri ya viwakilishi vya nafsi ili kujenga maana za kifalsafa na kisaikolojia. Miongoni mwa viwakilishi vinavyojitokeza kwa msisitizo ni "mimi". Miongoni mwa matumizi ya kiwakilishi hiki katika muktadha wa ubunifu wa kifasihi ni kuonesha migogoro ya utambulisho. Katika tamthiliya iliyotafitiwa, takriri ya "mimi" inadhihirika katika kauli za Shetani, Binadamu, Juma, Mtu 1, Mama, na Bibi. Inajitokeza kama mojawapo ya aina muhimu za ukiushi wa kisintaksia unaojengwa kupitia anafora[1] na epifora[2], ambapo kipashio kimoja cha lugha hurudiwa mara kwa mara katika nafasi tofauti za sentensi ili kuunda msisitizo wa kiitikadi na kiishara. Katika muktadha wa tamthiliya ya *Mashetani*, matumizi haya ya takriri yanavuka kazi ya kawaida ya mshikamano wa matini na kuingia katika eneo la kuvunja taratibu za mazungumzo ya kawaida, ambapo lugha hutegemewa kuwa na uchumi wa taarifa na maendeleo ya mantiki ya hoja. Hivyo basi, kurudiwarudiwa kwa "mimi" kunakuwa si suala la mtindo tu, bali ni mkakati wa kisanii unaobeba migogoro ya nafsi, mamlaka na utambulisho ndani ya jamii ya baada ya uhuru.

---

[1] Urudiaji wa neno au kirai kimoja mwanzoni mwa sentensi au vipashio vinavyofuatana ili kujenga msisitizo wa kimaana au kimtindo.

[2] Urudiaji wa neno au kirai kimoja mwishoni mwa sentensi au vipashio vinavyofuatana kwa lengo la kusisitiza wazo fulani.

Pia, mtandao mpana wa takriri ya "mimi" ulibainika katika miundo inayotumiwa na Shetani. Data inayofuata inadhihirisha:

SHETANI: Unanijua **mimi** nani?
**Mimi** Shetani.
Siyo jinni wala kuhani.
**Mimi** Shetani.
Uwezo wangu hauhifadhi.
Wema wangu hauhisabiki.
Ubaya wangu hausemeki.
*N*inajenga.
*N*inabomoa.
*Ni*natukuza.
*N*inadhalilisha nitakavyo.
**Mimi** ni nguvu na nguvu ni **mimi**.
**Mimi** ni uwezo na uwezo ni **mimi**.
Tazama miujiza. (*Anajibadilisha*) Sasa **mimi** nani? (uk. 1-2)

Katika dondoo hili, takriri ya "mimi" inaonekana katika nafasi tofauti za kisintaksia na kimaana, ambapo, wakati mwingine, inajitokeza kama kiima ("Mimi Shetani"), wakati mwingine kama sehemu ya kiima kilichopanuliwa ("Mimi ni nguvu"), na wakati mwingine kama kipengele cha muundo wa kiasmus ("Mimi ni nguvu na nguvu ni mimi"). Kwa mujibu wa Leech (1969), huu ni muundo wa kiasmus (*chiasmus*). Aina hii ya usambamba wa kimfumo hujenga athari ya kisanii kwa kusisitiza muundo wa lugha kama kipengele chenye uzito sawa na maana yenyewe. Hapa, badala ya sentensi kuwasilisha taarifa kwa mstari wa kawaida wa kiima-kiarifu, muundo unajipindua na kujirudia kwa namna inayomfanya msomaji au msikilizaji kuzingatia zaidi uhusiano wa nguvu kati ya vipashio vya "mimi," "nguvu" na "uwezo" kuliko maana ya moja kwa moja. Aina hii ya urejeleaji na kurudia wa vipashio vya lugha ni sehemu ya mikakati ya kimtindo inayovuruga matarajio ya kawaida ya msomaji, hivyo kumlazimisha kushughulika na muundo wa lugha badala ya mawasiliano ya

moja kwa moja (Leech na Short, 2007). Zaidi ya hapo, Mukarovsky (1977) anaeleza kuwa mchomozo hutokea pale vipengele vya lugha vinapotolewa katika matumizi ya kawaida na kupewa uzito wa kipekee wa kisanaa. Katika dondoo la Shetani, "mimi" haifanyi kazi ya kawaida ya kurejelea nafsi pekee, bali inakuwa alama ya mamlaka, nguvu na ubinafsi uliokithiri. Hivyo, takriri hii inajenga taswira ya mhusika anayejitambua kama kitovu cha nguvu na uhalisia wote, jambo linalovunja mipaka ya uhalisia wa kijamii na kuingia katika uwanja wa kiitikadi na kifalsafa.

Kwa upande wa mhusika Binadamu, takriri ya "mimi" inachukua sura ya mgogoro wa nafsi na kutokuwa na uhakika wa utambulisho kama inavyoonekana katika data inayofuata:

> BINADAMU: **Mimi** mtupu─**ngozi, damu na mfupa** (uk. 9)
> BINADAMU: **mimi─mimi** ndiye niliyejiangusha, siyo yeye─**mimi** (uk.11)
> Mtendaji ni **mimi**, **mimi** ni nani? **mimi─mimi** au **yeye─mimi**…… nilazime nisafri, safari ndefu, nikajitafute, nikajisake ili nijijue **mimi** nani? Ili ijue maana ya kitendo changu (uk. 12).

Katika mifano hii, kurudiwa kwa "mimi" hakujengi tu msisitizo, bali kunadhihirisha kuvunjika kwa umoja wa nafsi na mgawanyiko wa kiakili ndani ya mhusika. Muundo kama "mimi─mimi" na "yeye─mimi" unaonyesha kuvunjika kwa mipaka ya utambulisho, ambapo nafsi inajitazama yenyewe kwa macho ya mashaka na mgongano. Kwa mujibu wa tafiti za hivi karibuni katika Umtindo, kama zile za Simpson (2004) na Jeffries (2010), marudio ya kipashio cha nafsi katika matini za kifasihi huweza kuashiria mgogoro wa kiakili na kimaadili, ambapo lugha inakuwa kioo cha msongo wa ndani wa mhusika.

Katika muktadha wa Mtu 1, Mama, na Bibi, takriri ya "mimi" inajitokeza kama chombo cha kuonyesha ubinafsi wa kijamii na kiu ya maendeleo ya kimwili kama inavyoonekana katika data inayofuata:

MTU 1: "Mimi ninakwambia bwana, hakuna kitu kinachonifurahisha kama kumwona mwenzangu kapata…" (uk 44).
MAMA: **Mimi** ninataka nyumba ya peke yangu… Hakuna aliyekuwa … (uk 39).
BIBI: Na **mimi** nitamfuata huko huko Uzunguni atakokaa (uk 39).
JUMA: Wewe unaishi leo. **Mimi** ninaishi jana.
KITARU: Na wewe unafikiri, ndiyo wewe tu mwenye hadithi? Na **mimi** ninazo vilevile (uk. 56).

Katika mifano hii, takriri ya "mimi" inaonyesha ubinafsi unaojikita katika matamanio ya kiuchumi na kijamii, ambapo kila mhusika anajikita katika manufaa yake binafsi. Hapa, ukiushi hauko tu katika marudio ya kipashio cha lugha, bali katika kuonyesha kuvunjika kwa mshikamano wa kijamii na kuibuka kwa fikra za kibepari na ubinafsi. Kwa mujibu wa Blommaert (2019), matumizi ya kurudia nafsi katika matini ya kifasihi yanaweza kusomwa kama ishara ya miundo ya kijamii inayojengwa juu ya ushindani wa nafsi badala ya mshikamano wa kijamii.

**Ukiushi wa kutumia upinduzi wa sentensi**

Upinduzi wa sentensi ni kitendo cha kuunda au kupanga sentensi kwa kuvunja mtiririko wa kawaida wa Kiswahili sanifu, ambapo vipashio vya sentensi hupangwa kinyume na matarajio ya kawaida ya kisarufi au kimantiki. Katika mtazamo wa uchambuzi wa kimtindo, upinduzi huu si tu mkengeuko wa kiutendaji wa lugha, bali ni mkakati wa kisanii unaolenga kuchelewesha maana, kuongeza uzito wa tafakuri, na kuibua mchomozo kwa msomaji au msikilizaji. Hivyo, upinduzi wa sentensi katika *Mashetani*

unapaswa kueleweka kama sehemu ya ukiushi wa kimakusudi unaolenga kuunda athari ya kiakili na kihisia. Mfano mmojawapo wa upinduzi wa sentensi unaojitokeza katika *Mashetani* unahusisha kauli za Juma na Kitaru ambao wanasema:

| | |
|---|---|
| JUMA: | Kidonda cha mti kinasikikana harufu tu.<br>Hakionyeshwi. Aibu, aibu kubwa<br>(uk. 44). |
| KITARU: | Kama *Mashetani* hivi, kwa mfano (uk. 24). |

Sentensi hizi zinavunja mtiririko wa kawaida wa Kiswahili sanifu, ambapo taarifa ingetarajiwa kupangwa kwa mfuatano ulionyooka wa kiima, kiarifu na vijalizo vyake. Kwa mfano, badala ya mtiririko wa kawaida unaoweza kueleweka kwa urahisi, Hussein anaweka kiambajengo "Hakionyeshwi" katikati ya muktadha wa hoja kwa namna inayokatiza mtiririko wa mawazo. Hapa, lugha inapata tabia ya kusitasita, jambo linaloonyesha kwamba maana haijapangwa ili ipatikane kwa urahisi bali imesanifiwa ili kumlazimisha msomaji kusimama na kutafakari. Kwa mujibu wa Leech (1969), mkengeuko wa kanuni za kawaida za lugha huongeza nguvu ya kisanii ya matini kwa kuvuruga matarajio ya msomaji na kuamsha usikivu wake wa kiakili. Katika muktadha huu, upinduzi wa sentensi katika mfano wa "Hakionyeshwi" unafanya kazi ya kuchelewesha utambuzi wa maana, hivyo kuibua hali ya taharuki na uzito wa kisaikolojia. Msomaji hulazimika kuunganisha vipande vya maana vilivyotawanyika ili kupata ujumbe kamili, hivyo kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa maana.

Vilevile, sentensi ya KITARU: "Kama *Mashetani* hivi, kwa mfano" inaonyesha upinduzi wa mpangilio wa taarifa. Katika Kiswahili sanifu, tungetarajia muundo kama "Kwa mfano, kama *Mashetani* hivi," ambapo kiashiria cha mfano kingetangulia ili kuweka muktadha wazi. Hata hivyo,

Hussein anapindua mpangilio huu kwa makusudi, hivyo kuvunja utaratibu wa kawaida wa uwasilishaji wa taarifa. Upinduzi huu una athari ya kisemantiki na kiitikadi kwa sababu unafanya kauli kuwa ya kutafakari zaidi kuliko kueleza moja kwa moja.

Kwa mtazamo wa mtindo wa kimuundo, mkengeuko huu pia unaweza kuhusishwa na dhana ya Viktor Shklovsky ya ugenishaji, ambapo lugha ya kifasihi inafanywa kuwa ngeni ili kuifanya hadhira itazame jambo la kawaida kwa jicho jipya. Hivyo basi, upinduzi wa sentensi katika *Mashetani* unalenga kuondoa mazoea ya usomaji wa kawaida na kumlazimisha msomaji kuingia katika mchakato wa kina wa tafakuri. Hivyo, Hussein anatumia upinduzi si kama hitilafu ya lugha, bali kama mbinu ya kusukuma mbele maana fulani muhimu zaidi kuliko nyingine.

**Ukiushi wa kutumia udondoshaji na ukataji wa sentensi**

Miundo mingine katika *Mashetani* inadondoshwa na kudokezwa tu kwa sehemu fulani, ambapo baadhi ya vipashio vya sentensi huachwa wazi kwa makusudi na msomaji huachwa kukamilisha maana. Udokezo katika muktadha huu ni sehemu ya udondoshaji wa kimtindo unaohusisha kuondoa maneno au vipashio muhimu vya sentensi na kuacha mapengo ya kimawazo yanayohitaji kujazwa na hadhira. Kwa hiyo, udondoshaji haupaswi kueleweka kama upungufu wa kimawasiliano, bali kama mkakati wa kisanii unaojenga mwingiliano wa kiakili kati ya mtunzi na msomaji. Hussein anatumia mbinu hii kwa makusudi ili kuifanya hadhira isibaki katika nafasi ya kupokea taarifa tu, bali iwe mshiriki hai katika ujenzi wa maana.

Katika *Mashetani*, mara nyingi kuna uficho wa kimtindo, ambapo sehemu ya taarifa huachwa bila kukamilishwa kwa uwazi, jambo linalodokeza kuwa msomaji anatakiwa kuwa na uwezo wa kujazia maana iliyopotea. Hali hii inaweza kuwachanganya wasomaji wa kawaida, lakini kwa wasomaji makini huibua nafasi ya tafakuri ya kina na uchambuzi wa kimantiki wa maana fiche zinazojengwa.

Data inayofuata inaonesha kwa uwazi matumizi ya udondoshaji na sentensi zilizokatika.

> Kama ndege … vile… ndege, (uk. 2).
> Gashalazeri…t… was (uk. 4).
> maana… haiwezi kuwa …. Nikiamini hivyo ... basi yeye hakufa…! (uk. 9).
> Gash… Gasha… aaah
> Ukweli… acha yote hayo (uk. 17).
> Mama: Sasa ken…
> Juma uwongo… basi haram utaona (uk. 39).
> Mimi ninataka nyumba ya peke yangu … Hakuna aliyekuwa … (uk. 39).
> Kazi ya bure bwana haina … (uk. 40).
> Hata hai … (uk. 40).
> Mbona hatue... (uk. 40).
> Yaani ana... (uk. 40).
> Macho yanaona, akili inafikiri… Lakini…kiwiliwili hakihisi (uk. 42).

Katika mifano hii, tunaona kwamba sentensi zinakatika katikati ya mtiririko wa mawazo, au zinabaki na sehemu zisizokamilika ambazo zinahitaji kujazwa na msomaji. Kwa mfano, "Kama ndege… vile… ndege" inaacha pengo la kiakili linalomlazimisha msomaji kutafuta uhusiano wa kimantiki kati ya vipande vya kauli. Vivyo hivyo, "maana… haiwezi kuwa …. Nikiamini hivyo …. basi yeye hakufa…!" inaonyesha mgawanyiko wa mawazo unaovunja mtiririko wa kawaida wa hoja, na hivyo kuibua hali ya sintofahamu ya kimawazo.

Kwa mujibu wa Riffaterre (1978), udondoshaji katika matini ya kifasihi huunda mapengo ya kisemantiki ambayo humlazimisha msomaji kujaza maana iliyokosekana ili kupata ujumbe kamili wa matini. Hivyo, mapengo haya si udhaifu wa kisarufi, bali ni mbinu ya kisanii inayojenga mwingiliano kati ya maandishi na msomaji. Aidha, kwa mujibu wa Halliday (2014), udondoshaji unaweza kueleweka kama mabadiliko ya muundo wa taarifa, ambapo baadhi ya vipashio vya maana huondolewa lakini hubaki vinadokezwa kupitia muktadha. Hivyo, sentensi kama "Hata hai … (uk. 40)" au "Mbona hatue…. (uk. 40)" zinaonyesha kwamba maana haijakatika kabisa, bali imeachwa katika hali ya uwezekano wa kukamilishwa kupitia uelewa wa msomaji na muktadha wa matini.

**Ukiushi wa kutumia urefushaji wa kauli**

Urefushaji wa kauli ni mojawapo ya aina za ukiushi wa kisintaksia zinazojitokeza katika tamthiliya ya *Mashetani*. Hussein anautumia mkakati huu kwa kupanua wazo moja kupitia mbinu mbalimbali kama vile urudiaji wa maneno, matumizi ya visawe na miundo ya kisintaksia inayorejelea wazo lilelile kwa namna tofauti. Kwa mtazamo wa kimtindo, urefushaji huu unakiuka kanuni ya uchumi wa lugha. Pia, huongeza uzito wa maana na athari ya kisanaa. Kwa hiyo, urefushaji unakuwa mbinu ya kisanii inayolenga kuimarisha msisitizo wa kimaana na kuunda athari ya kihisia na kiakili kwa hadhira.

Katika tamthiliya iliyotafitiwa, Hussein anatumia maneno na virai vinavyofanana kimaana lakini yaliyo tofauti kimuundo ili kujenga mkazo wa kisemantiki kama inavyoonekana katika mifano inayofuata.

> Amekufa. *Nimemuua*! *Nimemuua*! *Nimemuua* au alitaka *nimuue*? (uk. 8).

> Ina maana kuwa huu wote ulikuwa mchezo tu. *Stihizai*. *Shere*. Ngoja, ngoja (uk. 9).
> Hilo siwezi kuamini, haliaminiki. Kuamini hilo ni kuamini kuwa yote aliyosema ni kweli-kuwa mimi… hata kidogo… kivuli…? Haiwezekani (uk. 11).
> Mimi nimeota manyoya, mzee ameota manyoya, kila mtu na kila kitu kimeota manyoya, manyoya mengi, mengi sana (uk. 48).

Katika mifano hii, urefushaji wa kauli unajengwa kupitia mbinu mbalimbali, hususan urudiaji wa maneno, matumizi ya visawe na kurejelewa kwa wazo lilelile kwa miundo tofauti ya kisintaksia. Mbinu hizi haziongezi taarifa mpya, bali huongeza uzito wa maana, msisitizo na athari ya kihisia katika matini. Kwa mfano, katika "Amekufa. Nimemuua! Nimemuua! Nimemuua! Nimemuua au alitaka nimuue?" tunaona msukumo wa kihisia unaojengwa kupitia marudio yasiyo na nyongeza ya taarifa mpya, bali yanayoimarisha mshtuko na mkanganyiko wa mhusika. Hali hii inaonyesha kuwa lugha inatumika zaidi kama chombo cha hisia kuliko chombo cha mawasiliano ya moja kwa moja. Aidha, matumizi ya maneno "shere" na "stihizai" katika muktadha mmoja hayaleti taarifa mpya bali yanapanua wazo la kejeli kwa kulirudia kwa namna tofauti ya kimtindo. Vilevile, marudio ya kauli kama vile "kuamini, haliaminiki; kuamini hilo" yanaonyesha jinsi wazo moja linavyorejelezwa kwa miundo tofauti ili kuimarisha hisia ya mashaka na mgongano wa kiakili. Hii ina maana kuwa urefushaji hapa si kuongeza taarifa, bali ni kuongeza uzito wa kiathari wa ujumbe.

Kwa mujibu wa Halliday na Hasan (1976), urudiaji wa vipashio vya lugha huchangia katika kuunda mshikamano wa matini (*cohesion*) na kuimarisha muunganiko wa dhamira ndani ya kazi ya kifasihi. Katika muktadha wa *Mashetani*, urefushaji kupitia urudiaji unafanya kazi ya kuunganisha hisia

na mawazo ya wahusika, huku ukisisitiza hali ya kiakili ya msongo, mashaka na mgogoro wa ndani.

Aidha, kwa mtazamo wa Nadharia ya Umtindo ya Leech, urefushaji unaweza kueleweka kama aina ya mkazo wa kimtindo unaovunja matarajio ya uchumi wa lugha. Badala ya sentensi fupi na za moja kwa moja, Hussein anatumia marudio na visawe vinavyozunguka wazo moja ili kulifanya liwe na uzito wa kipekee. Kwa mfano, kauli ya "Hilo siwezi kuamini, haliaminiki" inaonyesha mgongano wa ndani wa mhusika unaojengwa kupitia kurudia kwa wazo la kutoamini, jambo linaloongeza kina cha kisaikolojia.

Vilevile, miundo kama vile "**Mimi** ni nguvu na nguvu ni **mimi**" (AB BA) na "**Mimi** ni uwezo na uwezo ni **mimi**" (ABBA) inaonyesha matumizi ya urudiaji wa kimuundo unaojenga mdundo wa kimawazo na msisitizo wa kiitikadi. Miundo hii haibebi tu maana ya moja kwa moja, bali inajenga picha ya mhusika anayejitambulisha kwa kujirudia na kujifunga ndani ya nafsi yake. Hivyo, urefushaji hapa unafanya kazi ya kuimarisha taswira ya mamlaka, ubinafsi na nguvu ya kiitikadi ya wahusika.

**Hitimisho**

Uchambuzi uliofanywa katika makala hii umebainisha kuwa ukiushi wa kisintaksia katika *Mashetani* si ajali ya kiisimu wala udhaifu wa kiuandishi, bali ni mkakati wa kimakusudi wa kisanii. Utaratibu wa kawaida wa uundaji wa sentensi na mfuatano wa maneno unakiukwa kwa namna inayoibua mshangao na kumlazimisha msomaji au mtazamaji kutafakari kwa kina maana inayojengwa. Miundo iliyopinduliwa, sentensi zisizo kamili, pamoja na urudiaji wa maneno na miundo ya kisentensi hujitokeza

kwa wingi kama mbinu ya kuunda mchomozo unaovuruga matarajio ya kawaida ya lugha. Urudiaji wa miundo ya kisintaksia una nafasi mahususi katika kujenga athari ya kukejeli na kuimarisha kinaya kinachoelekezwa katika mfumo wa ukoloni mamboleo na migongano ya kitabaka. Kwa njia hii, muundo wa sentensi hauwi chombo cha mawasiliano tu bali hubeba uzito wa kimaudhui na kifalsafa. Hivyo, muundo na ujumbe vinafungamana kwa karibu, kiasi kwamba, kuyatenganisha kunapunguza upeo wa uelewa wa tamthiliya yenyewe.

Kutambua ukiushi wa kimakusudi katika kazi ya mtunzi kunadhihirisha ustadi wake wa kisanaa na uwezo wake wa kutumia lugha kama chombo cha uchunguzi wa kijamii na kisaikolojia. Bila uchambuzi wa namna hii, ni vigumu kwa msomaji au mhakiki kuibua kwa kina dhamira na falsafa iliyofichwa ndani ya tamthiliya. Hata hivyo, hoja za baadhi ya wahakiki wanaomlaumu Ebrahim Hussein kwa kutumia mbinu zinazodaiwa kuwa tata au zinazoweza kuwatenga wasomaji hakuwezi kupuuzwa kabisa. Ukweli ni kwamba mbinu zake zinahitaji hadhira yenye utayari wa kuchunguza na kutafakari zaidi. Hata hivyo, ugumu huo haupaswi kufasiriwa kama udhaifu, bali kama mkakati wa kimtindo unaolenga kuinua kiwango cha usomaji na tafakuri katika tamthiliya ya Kiswahili.

## Marejeleo

Blommaert, J. (2019). *Sociolinguistics of Globalization*. Cambridge: Cambridge University Press.

Burke, M. (Mhar.). (2021). *The Routledge Handbook of Stylistics*. London: Routledge.

Carter, R. & Stockwell, P. (2022). *The Language and Literature Reader: Style and Stylistics*. London: Routledge.

Cluysenaar, A. (1976). *Introduction to Literary Stylistics*. London: Batsford.

Halliday, M. A. K. (2014). *Halliday's Introduction to Functional Grammar* (Toleo la 4). London: Routledge.

Halliday, M. A. K. & Hasan, R. (1976). *Cohesion in English*. London: Longman.

Jakobson, R. (1960). Closing Statement: Linguistics and Poetics. Katika T. A. Sebeok (Mhar.), *Style in Language* (kur. 350-377). Cambridge, MA: MIT Press.

Jeffries, L. (2010). *Critical Stylistics: The Power of English*. Basingstoke: Palgrave Macmillan.

Leech, G. N. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman.

Leech, G. & Short, M. (1981). *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to English Fictional Prose*. London: Longman.

Leech, G. & Short, M. (2007). *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to English Fictional Prose* (Toleo la 2). Harlow: Pearson Education.

Mukarovský, J. (1977). The Word and Verbal Art. Katika J. Burbank & P. Steiner (Wahar. na Watafs.), *The Word and Verbal Art* (kur. 1-30). New Haven: Yale University Press.

Mukarovsky, J. (1990). Standard Language and Poetic Language. Katika P. L. Garvin (Mhar. Na Mtafs.), *A Prague School Reader on Esthetics, Literary Structure, and Style* (kur. 17-30). Washington, DC: Georgetown University Press.

Mwansoko, H. J. (1991). *Mitindo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: University of Dar es Salaam Press.

Ngara, E. (1982). *Stylistic Criticism and the African Novel*. London: Heinemann.

Riffaterre, M. (1978). *Semiotics of Poetry*. Bloomington: Indiana University Press.

Shklovsky, V. (1965). Art as Technique. Katika L. T. Lemon & M. J. Reis (Wahar. na Watafs.), *Russian Formalist Criticism: Four Essays* (kur. 3-24). Lincoln: University of Nebraska Press.

Simpson, P. (2004). *Stylistics: A Resource Book for Students*. London: Routledge.

Van Peer, W. (1986). *Stylistics and Psychology: Investigations of Foregrounding*. London: Croom Helm.